kuwakilisha eneo fulani kama mbunge ama councillors. Kwa hivyo naomba hizi nafasi za wambunge maalum zipewe walemavu. Kwani pia ni chache na pia tunaweza kuwakilisha kila mmoja, awe mlemavu ama siye mlemavu. Kwa hivyo naomba tupewe hizo nafasi kwa sababu ni chache na zinatufaa. Kwa vifaa vya walemavu kama hivi wheel chairs ama crutches zitolewe ushuhuru kwa sababu zimekuwa bei ghali sana. Wengine wetu tunapowaona walemavu wakitembea kwa kujivutia chini kwa sababu hawawezi kizi afford, yaani tuseme kama crutches ama wheel chairs iko na bei ghali sana. Nangingomba serikali atupatie hizi vifaa bila malipo. Pia naomba mashirika ya walemavu yasimamiwa na walemavu wenyewe. Kwa sababu tunaona wale wenye wako kwa mashirika kama hayo ambao singetaka kuwataja yapo lakini wanasimamiwa na wenye si walemavu na kwa hivyo wanawatenga sana walemavu ambao wanafaa kuwawashiriki katika mashirika hayo. Si kuwa na mengi sana, asante sana kwa kunipatie nafasi hii. Kwa majina tena ni Rose Wangari.

**Com. Zein:** asante sana Rose. Atakuletea register uandike register kwamba umetoa maoni kwenye chumba cha katiba.

**J oel Kiandiko:**

**Com: Zein:** pole sana kwa kuita jina vibaya.

**Joel: in vernacular**

**Interpreter:** nimekuja hapa kutoa maoni yangu

**Mr Joel:**

**Interpreter:** juu ya katiba

**Mr Joel:**

**Interpreter:** nataka kuzungumzia juu ya wake ambao wamekwisha kufiwa na ume zao.

**Mr Joel:**

**Interpreter:** nao wanashida kama hizi

**Mr Joel:** shida za mashamba

**Mr Joel:**

**Interpreter:** wananyan' ganywa mashamba yao kwa sababu waume wao hawako.

**Mr Joel:**

**Interpreter:** ndio tunataka kusema juu ya katiba

**Mr Joel:**

**Interpreter:** kama katiba itageuza mambo kama hayo

**Mr Joel:**

**Interpreter:** mabibi hawa ambao hawana mabwana wamenyan' ganywa mashamba yao

**Mr Joel:**

**Interpreter:** mtu kama mimi ni mmoja baba hayuko, mama hayuko

**Mr Joel:**

**Interpreter:** nimehangaishwa sana na hawa matajiri.

**Mr Joel:**

**Interpreter:** hata sasa wakati kama huo ninafanya kesi kwa shamba langu



**Mr Joel:**

**Interpreter:** kwa hivyo katiba

**Mr Joel:**

**Interpreter:** wale watu ambao wamezunguza juu ya mambo yetu ya kiasili

**Mr Jacob:**

**Interpreter:** ningependa ya kwamba ile kiapo ya zamani au kaiurubo irudishwe

**Mr Joel:**

**Interpreter:** hata kama wakati huu ni mchristo

**Mr Joel:**

**Interpreter:** naninajua yale maamuri kumi na mbili

**Mr Joel:**

**Interpreter:** naona kwamba ni wale wamesoma ndiyo wanataka kunyan'ganyawale hawajui mali zao.

**Mr Joel:**

**Interpreter:** jambo lingine ni hili

**Mr Joel:**

**Interpreter:** mambo ya masomo

**Mr Joel:**

**Interpreter:** nimewasomesha watoto wangu wote sana lakini hakuna hata moja ameandikwa.

**Mr Joel:**

**Interpreter:** wale ambao wamesomeshwa ni wamasomo ya chini sana.

**Mr Joel:**

**Interpreter:** wale ambao wamesoma sana hawajajiriwa

**Mr Joel:**

**Interpreter:** kwa hivyo wale ambao wamesoma sana wanaangaishwa sana

**Mr Joel:**

**Interpreter:** hata kwa mfano wale wenye wako hapa lakini ni walemavu pia wao wamesoma sana.

**Mr Joel:**

**Interpreter:** nasema ni asante sana

**Naman Ndereva:** asante sana kwa wale ambao wametumwa kwa sababu ya kugeuza katiba. Mimi naitwa Nama Ndereva na kwetu ni hapa Mbeere. Na mimi nimetumwa na watu wa --- ambaye wamejitolea kufanya kazi yao. Na hawa watu walikaa chini na wakaandika mambo ambayo inahusu ugeuzi wa katiba. Kwa hivyokulingana na vile ambao mambo imearibika, kwa sababu ya mambo machache tu. Kama upande wa utawala, kutoka kwa village elder, assistant chief, chief wawe wakiandikwa na raia kwa kutumia njia ya mlolongo. Kwa sababu zamani hakukuwa na mambo mengi kama wa sasa. Kwa vile ikiwa ni chief au assistant chief alikuwa anajua tu hawezi tumia nguvu vile wanatumia kwa sababu anajua ameandikwa na watu. Na alikuwa akiangalia mambo ambayo inahusu watu ambao anaongoza. Mambo ya pili

inahusu mashamba. Kulingana na mila ya watu wa mbeere, kwa zamani hakukuwa na unyan'gaji mkubwa sana juu ya shamba. Kwa sababu ikiwa watu wameanza kupigania mashamba walikuwa wanakaa tu chini wanawambia kama mnapigania, lazima mtakula kiapo. Na wakila hiyo kiapo haikuwa michezo kama ukiwa unyan'ganya mwingine shamba lazima utakufa. Nakwa sababu ya wakati huo watu walikuwa wanakunywa kiapo ama ukijua unyan'ganya mwingine unawacha halafu unawachia mwenyewe shamba lake. Na wakati huo mambo ilikuwa si kama wa sasa. Ilikuwa mambo tu mazuri sana haikuwa na taabu nyingi sana. Ya tatu, hapa hata vile mnasema mambo ya ugonjwa wa ukimwi umeingia, kwa sababu ya mambo kushakuwa mbaya. Kama wakati wetu mbere kudunga msichana mimba wazee walikuwa wanakaa chini, wawe wazee wawili. Wanaitana wanazungumza, kama ukiwa hutaki kuo msichana wangu, unatoa ndume nne na ile inaitwa dhenge nne halafu anaambiwa na hawa wazee usirudie hiyo maneno. Na ikisema haki kama vile unajua hiyo ndume iko na ukutoa hiyo yote ulikuwa unaona unahamgaisha baba yako sana. Na hiyo mambo ya mimba haikuwa mingi sana kama ya sasa. Hata ugonjwa haikuwa mingi kama ya sasa. Kwa hivyo mimi kitu naomba hiyo kitu irudishwe ili hata hii mambo ya ukimwi ikwishe. Mambo ingine ni mambo ya kama sasa nimeoa bibi yangu au watu wameoa mabibi yao. Watu wengine zamani hawakuwa na mambo mengi sana. Kama ukiwa unaenda mke wangu, wazee wanakaa chini halafu unaitwa. Unaambiwa kwa sababu umefanya aibu na umefanya bibi ya huyu mtu aende njia ambao hajilikani mtu alikuwa anaambiwa atoe n'gombe mbili na ndume mbili. Hayo mambo kulingana na kimbere wetu mtu hawezi kurudia mambo kama hayo. Mambo ya nne, mambo ya mashamba mahali ambapoo mtu amekaa zaidi ya miaka kumi. Kwa sababu mtu hawezi kaa pahali bila kujua anakaa kwa sababu gani. Sasa hiyo anakaa hakuenda kuomba mtu mahali ya kukaa. Kulingana na kimbeere yetu kama shamba ni langu, mimi naenda tu kwako kama maswali nakuja kuomba. Sasa vile unasikia watu wakisema kama upande wa kanyobora kwa sababu hiyo ilikuwa inaitwa wealth na hapo ndiyo mambo imearibikia mambo ya kanyobora na kawsengero area. Kwa sababu tu wale wenye wako na pesa ndio wananyan'ganya watu mashamba yao. Na wakati walikuwa wakienda huko hakuna mtu ambaye alikuwa akiomba mtu mahali ambapo anaenda kutengeneza shamba lake. Na hawa watu walikuwa wanapelekwa huko na serikali. Mtu anaenda kukata mahali anataka anakatazwa na mwingine. Kwa hivyo hiyo ndio tunasema kwamba ili tumalize hii mambo ya watu ya matumbo kubwa kubwa kukula wale wengine, kiapo irudishwe na watu wawe wakipewa mashamba kwa sababu huyo mtu alikuwa amekaa hapo kama 60 years na hana mahali ambapo atapeleka hawa --- zake. Mambo ya uchumi Kulingana na wakati huu mambo ya uchumi umekuwa mabaya sana kwa sababu mambo imekuwa – kiatika ministries . Ministries imekuwa nyingi sana. Kama ilikuwa un--- upande wa agriculture haikuwa na ministries nyingi sana, na haikuwa na mambo mengi sana. Na ukiona wakati huu kwa sababu ministry imekuwa mingi sana. Ndio Kenya iko na mambo mabaya sana ambayo hawezi kuzisaidia kwa sababu ya kuwa ministry nyingi. Kwa hivyo tunaomba hiyo ministry serikali aangalie ili mambo mambo ya serikali isiwe mengi sana kwa sababu akiangalia hiyo ministry kama ya zamani, mambo yao itakuwa mazuri sana.

**Com. Zein:** Ndereva muda wako umekwisha na nishakuongezea dakika ingine moja. Umebakisha maneno mangapi?

**Ndereva:** moja tu

**Com. Zein:** haya malizia

**Mr Ndereva:** Mambo ingine, kama hii ya hospitali nimesikiamtu mwingine amezungumza. Kulingana mambo ya hospitali

tunaomba serikali yetu iangalie sana kwa sababu watu wengine hawajiwezi hata kidogo. Wengi wamekufa kwa sababu hawana pesa. Hata wakienda kwa hospitali bila pesa mtu anafariki tu kwa sababu hana pesa.

**Interjection:** ungependekezo gani mzee wangu?

**Mr Ndereva:** iwe kama zamani, bure. Kwa hivyo sina mengi isipokuwa hayo tu.

**Com. Zein:** asante sana mzee --- tafadhali uende uandike jina pale kwenye register na utoe memorandum na hiyo maandishi tutayasoma.

**Eustus Nthamburi:** kwa majina naitwa Nthamburi Eustus. Kwa vile maoni yangu nimeonelea ya kwamba naingilia tu kwa kimbere straight. We have our customs that bind us to have what really bound us to be mbere people. That is we had the council elders in their old times and we would still like to have the same from sub-location level, division level upto district level. These councils will care for cultural disputes regardless these are domestic or the outcry in the country. They would look for that. These same kind of people should at least men or women of a good reputations not --- because there are those who do not care what they do and when they do I and therefore according to my view is that there should be people of a good age that's around 60 or 70. Marriages. Mbeere people have had and even now have traditions of





if I have to make marriage at anyone's home I should pay a dowry of seventy goats, one bull and one he-goat. That is to ensure there is commonness in marriage as needed in kimber form. There are also areas that kuna hali ya karobo ambayo ilikuwa lazima baba, mama wakunywe na kila mtu katika hiyo jamii hiyo waweze kujumuika nayo. Hiyo ni kumanisha everybody knows surely someone is getting married to this lady and from this and this area. We come to discipline, if for instance any of the boys impregnated any girl there was to be a penalty. Infact it was painful for any family to produce four bulls and four he goats and therefore for that point of discipline everyone was aware he didn't actually misuse his time or property in that form. And if there was no marriage at all after the impregnation of the girl, there was also this measure taken towards the gentleman. That was to take an oath not to bewitch the girl or to bewitch the family. Then I switch to land. It is to my feeling that if land bonds be shifted to the chiefs and not the Dos for any formalities at all. This would otherwise determine better times on money or time on whoever is concerned to have at least express himself towards his peace of land if any dispute at all. By this I am referring back to the council of elders even in the division and the district. With that one I get to the appeal if any one wants to get the appeal on his land, should he be given enough time and not the 14 days? I preferred because he has used his money and either all his possession why one not be given at least three months to look for the demands for the appeal. One should be given three months to look for the necessary items for appeal. You excuse me for a moment sir.

**Com. Zein:** Hiyo ni kuonyoksha. Hiyo kengele ni ya kukuwon tu ndio umalizie. Nakupa fursa umalizie. Uko na points kama ngapi imebaki?

**Mr Nhtamburi:** Points mbili tu but very precise.

**Com. Zein:** Malizia mzee

**Mr Nthamburi:** asante. I come now again to the area of retirement. This one I think the government should retire people at 60s and take care on their medication all the time because by this time I hope everyone is really ruthless to go here and there looking for medication but the government should this time take more care on retirees. Education.

Referring to our present system of education in Kenya, if we look at Kenya, Uganda, Tanzania we find that if we had not been very selfish our education in form four is useless because it shows that if in Uganda, they have their aggregate to the university, Tanzania the same. Our students from form four can't join any of the universities, what are we worth in this education? So we are bound to remain without furthering our education anywhere as today's education in east Africa for which we lag very much behind. Nevertheless, I call also to this other area of teachers recruitment on teacher training. The teacher training requirement these days otherwise to a few days seen in the papers that they would like to harass the parents. Most of our children really have Ds and even Es in mathematics. Having these Ds and Es in mathematics that the ministry needs D+, I wish the constitution defines exactly what should anyone be as early as now because most of our children have to be castled from teacher training because of only one subject and that is mathematics other than taking it as a general. If we have an aggregate of D, let our children get to the teacher training and let them enjoy the offer as it has been there before. Thank you.

**Com Zein:** asante sana mzee Nthamburi. Tafadhali andika jina lako kwenye register. Anayefuatia ni Florence Muite. Karibu mum, karibu.

**Florence Muite:** asante. Nitaanza na maoni yangu. Ya kwanza, nataka basic education iwe free au ya bure kwa watoto wote katika shule za public. Cost sharing afadhali itolewe kwa mahospitali ya government ikuwe bure. Violence on women itolewe, hatutaki hiyo. Hata land wanawake wapewe au wapewe rights on it. Watoto wapewe hakli yao. Citizenship ya wanawake, mwanamke akienda nje ya Kenya anaonekana yeye sio citizen wa hapa. Tunataka hata akienda yeye akuwe citizenship ya hapa. Resources kama huku kwetu tunataka tupewe stima na STD pia tupewe. Mtu akifikisha 60 years akiwa wa Kenya tunataka government ikiwa ikimwalia, akiwa analipwa na government. Kwa sababu saa yote sisi wote tunawapea kura lakini hawatuangalii. Akifikisha 60 years aangaliwe na government. Kulingana na executive the PC should be out kwa sababu hata wananchi wengi hawamjui ikuwe kutoka kwa president ni DC, DO, chiefs na assistant chiefs. Msichana akidungwa mimba na mvulana kuna n'gombe tunatolewa kama nne na mbuzi nne lakini huyo akikataa na uende kotini hiyo n'gombe ni shilingi ishirini pekee yakeau mbuzi shilingi ishirini. Tunataka ilipwe kulingana na vile tuko. Sio shilingi ishirini, na hiyo tumewapatia asanteni.

**Com. Zein:** asante sana bi. Florence. Anayefuatia ni Munyi Muthega. Mpe tu mzee hapo hapo.

**Munyi Muthega:** in vernacular

**Translator:** asante bwana commissioner.

**Mr Munyi:**

**Translator:** viongozi wote

**Mr. Munyi:**

**Translator:** nimeletwa hapa na shida.

**Mr Munyi:**

**Translator:** wakati alikatwa mguu huu

**Mr Munyi:**

**Translator:** yeye haoni vitu za kumsaidia.

**Mr Munyi:** wakati wanakuja wanaambiwa watasaidiwa, wanarudi kwa furaha wanangoja ngoja na hawapati.

**Mr Munyi:**

**Translator:** nahapati usaidizi

**Mr Munyi:**

**Translator:** kwa mfano akipeleka mtoto shule

**Mr Munyi:**

**Translator:** wakati mwingine haijulikani mtoto wa masikini.

**Mr Munyi:**

**Translator:** anasikitika sana kwa sababu anauliza sasa atatoa pesa wapi

**Mr Munyi:**

**Translator:** anasikitika sana

**Mr Munyi:**

**Translator:** na anaona kwamba kuna watu wa usaidizi ambao wanawachukua wakiwa walemavu

**Mr Munyi:**

**Translator:** sasa walingoja

**Mr Munyi:**

**Translator:** wanaona kwamba hawasaisii

**Mr Munyi:**

**Translator:** wanasema wanasikia kwa masemo tu ndio wanasaidiwa

**Mr Munyi:**

**Translator:** lakini akingoja anaona kwamba ni udanganyifu

**Mr Munyi:**

**Translator:** anasema amekuja kuona kama kuna watu anaweza kupata msaada aweze kujenga kanyumba kidogo ambacho anaweza kumsaidia

**Mr Munyi:**

**Translator:** yeye anatoka karibu na pahali panaitwa Kiaga. Pahali hakuna maji, wanawake wanapata shida sana kwa mgongo kuenda kuchukua maji mbali. Wamekuwa wakiambiwa kwamba watapata maji, wanaangaika tu

**Mr Munyi:**

**Translator:** kwa mfano mtu akienda jhospitali anaulizwa alipe pesa nyingi na anasumbuka sana kwa sababu pesa ni nyingi

**Mr Munyi:**

**Translator:** anasema kama ingewezekana wangukuwa wakisaidiwa watibiwe halafu hata kama ni kutibiwa na kuenda nyumbani ndiye atafute ile pesa alete.

**Mr Munyi:**

**Translator:**



Aanasema kwamba anaomba sana anawatafadhalisha sana Mungu awasaidie ili muweze kuwasaidia. Yeye sasa hata hana nyumba. Nyumba yake iliochomeka

**Mr Munyi:**

**Translator:** hata nguo hizi anazovaa sasa ni watu tu ndio wamemchangia

**Mr Munyi:**

**Translator:** anaomba msaada kutoka kwenu. Mungu asaidie nyinyi ili muweze kusaidia wale ambao hawajiwezi

**Mr Munyi:**

**Translator:** nasema kwamba hata ya kwamba mmewaita ili muweze kukwasaidia ni asante sana

**Mr Munyi:**

**Translator:** Mungu awasaidie akuweke siku nyingi, asante sana.

**Com. Zein:** asante sana tafadhali mpelekeni register pale mzee aandikishwe jina. Asante sana mzee

**Denisio N. Njagi:** asante sana bwana commission. Jina langu ni Denisio N Njagi. Jambo la kwanza , yaani kutoa maombi ni kwamba sisi wambeere tungetaka hiyo mambo ya zamani iwe haitupuliwi mbali hasa. Kama vile wengi wetu wamesema kama wale wameongea hapo mbeleni mambo ya customsry laws. Hiyo ni kutu ambacho ingechukuliwa kamaq kitu ya muhimu sababu inazuia mambo mingi ama uizi mwingi isionekane hapa. Jambo lingine ni vile mambo ya mashamba. Kunao wale wenye wako na mashamba kubwa kuliklo wale wengine. Wale wako na mashamba kubwa kushinda wengine ingefaa wale hawana wafikiriwe jabulaha. Sababu wengi hawana wamezaliwa tangu mashamba igawanywe. Tuseme kama upande zingine kama mwea, huko sababu ni ---- (naudible) hiyo wale hawana mashamba ndio wangepaa wapewe hiyo mashamba. Wafikiriwe kwanza. Jambo lingine ni vile mambo ya hospitali. Watu wakipelekwa hospitali pengine mtu aage dunia huko hospitalini na apelekwe mortuary,huyu mtu anakuwa ati mtu wa kulipiwaa pesa na saa ile sio mtu wa kuja kufarikimwenyewe tena. Hiyo mambo ingefaa ifutuliwe. Kwa sababu huwa inagarimu watu wengi sana wanakosa pesa. Hata watu wanaogopa kupeleka watu wao hospitali sababu wakiaga wakipelekwa kule itagarimu yule mtu mwingine na hana chochote.Na kule kupeana garama kama vile watu wakiwa hospitalini, watu wengi wanaogopa sana kwa sababu hawana chochote.Kwa hivyo ingefaa mahospitali ziwe za free ikiwezekana kama vile ilipokuwa hapo mbeleni. Pia mambo ya mashule za msingi ikifaa serikali ifikirie iziondoshe malipo yoyote. Sina mengi nitakomea pale. Asanteni.

**Com. Zein:** asante sana bwana Njagi. Tafadhali sign register yetu kwamba umetoa maoni yako. Asate sana

**Joseph N Ileri:** Mimi kwa majina ni Joseph Nyaga Ileri. Maoni yangu ni kwamba mimi ni wa Karo na hapo hapo mimi ni mtu ambaye ako na ulemavu, yaani ni mtu asiyeona. Kwanza nitazungumza juu ya walemavu pamoja na ulemavu nilionao. Nimewaambia mimi ni mtu asiyeona. Napenda kusema ya kwamba watu waliowalemavu wako nashida nyingi sana. Kwa mfano nitawambia kwamba mimi tangu nikae kama miaka tano hivi sita uliyopita, tumekumbana na maatatizo mengi sana. Na hiyo ni kusema hata wengi kama mimi hata kama walikuwa wakifanya kazi pahali wakiritaya huwa wako na shida nyingi. Kwa mfano mtyu mlemavu anaweza kutafuta jinsi anavyoweza kujisaidia.kama ni kabiashara hivi. Utaona biashara yake haiwezi kustawi sana kwa sababu ile ishiundaji ulioko na mamboa mengi sana. Utaona aznafuatwa sana kama ni local authorities wanamwangaisha sana.Ningeomba mtu mlemavu akijitahidi kuweka kabiashara kake tafadhali

sana katiba itakayotengezwa itengeze sheria ama kitu kama sheria hivi ya kuwalinda, hivi kwamba asifuatwe sana kwa vile hata kule anatoa bidhaa wakati mwingine hawezi kufika wakati ufaao. Kwa hivyo ningepomba ikiwezekana hii mambo ya licence iwe exempted ama iondolewe kwa walemavu. Nikiwa hapo hapo nitasema ya kwamba mlemavu ako na shida kama nilivyosema ya kwanza. Wengi tuna watoto na wanaenda shule kama watoto wa watu wengine. Mlemavu ambaye hana njia ya kujisaidia, anafuatiliwa ama anakabiliana na matatizo kama wale watu wengine. Ningepomba watoto wa walemavu waangaliwe, kwenye elimu waweze kuhudhuria elimu bila kutatizwa ikiwezekana. Hapo hapo ningesema ya kwamba mtu mlemavu anaweza kutumjia pesa nyingikwa mfano kama mimi niliporitaya, nimetumia pesa nyingi sana kupeleka watoto colleges na hata wakimaliza bao hawapati kazi. Sasa kile ninacho kidogo ndio tunasukumania nao hata sasa nimefrisika. Hiyo ni mfano kwa sababu najua kuna wengi kama mimi. Kwa hivyo tafadhali, watoto wapate kazi wakitoka shuleni. (*loss of few words*) Hatujui kama watafaidika na kupata kazi. Kwa hivyo mambo hayo yaangaliwe na katiba ijayo. Hapo hapo nikizungumzia juu ya elimu, na hii si kwa walemavu pekeeyao. Ni kwa watoto wote kwa sababu wote ni wqa Kenya. Mimi ningepeneda kuomba kama training institute kama training colleges za walimu, za medical ama zile zingine, tafadhali ziwe kama za zamani. Zisitoshwe malipo yoyote kwa sababu pesa siku hizi imekuwa shida sana karibu watu wote hata wasio walemavu. Kwa hivyo ile ombi ningepomba hili ni kwa watu wote, watoto wote ni wa kienya. Tafadhali na elimu vile vile kuanzia msingi kuenda juu tafadhali iangaliwe ikiwezekana iwe ya bure. Halafu nikitoka hapo niongee kama raia ya kawaida. Nizungumze juu ya wambuge. Ningepomba ya kwamba wananchi ya eneo Fulani ikiwa watafanya makosa wachague mtu asiyewasaidia, ningepomba sheria ijao itengeneze kama sheria hivi. Ikiwa wananchi watalalamika mjumbe w3ao hafanyi kazi hawasaidii sawasawa aitishwa uchaguzi mwingine uchaguliwe mtu mwingine ambaye anaweza kusaidia watu hawa. Na huyu mtu asikubaliwe kushiriki tena kwenye huu uchaguzi. Nikiwa hapo hapo, ningezungumza tena juu ya vyama vya kisiasa. Tukisha fanya uchaguzi kile chama kitachukua uongozi tafadhali ningepomba kwa katiba ijao ilazimike kuchukua majibu ya kulete maendeleo pahali popote. Hata kama ni zile sehemu wanaona hawakupata kura nyingi tafadhali maendeleo yaemde mahali popote kwa sababu Kenya ni moja. Hata kama kuna wapinzani sehemu Fulani Fulani hizo sehemu haziwezi kiukatwa Kenya ziiondolewe zipelekwe pahali pengine. Ziko ndani ya Kenya na itakuwa hivyo milele kwa hivyo ninaomba maendeleo ipelekwe kila pahali ikiwezekani hata kama ni huko kwenye upinzani. Nikizungumzia kidogo hasa sehemu kama hii yetu tuko nyuma na mambo mengi. Ukiangalia nguvu za umeme zinatoka hapa kiambere na ukiangalia ni sehemu ndogo tu ambao imefika. Ukiingia huko ndani ni jijini kama huko kwa rerema ama Kiagambua, Mangose kufika huko Ngarwereru. Karibu na hapo stima imetoka hakuna mwangaza hakiuna sitima. imefanywa kuzunguka tu. Sasasehemuzingine zimewekwa katikati kama bakuli, hazina maendeleo ya namna hiyo. Telephone, simu mtu akiwa na jambo la dharura hawezi kufanya uwasiliano ili aweze kupata mtu wa kumsaidia. Kwa mfano ugonjwa unaweza kuja usiku na hakuna pahali unaweza kukimbia hata kama ni kupiga simu----- (**inaudible**). Hata kama ni jirani yako unajua ako na simu unaweza kuwasiliana na yeye ungempigia kama ingelikuako. Lakini unaendelea tu mpaka wakati amaungu atakusaidia upate labda mtu mwenye baiskeli akubebee huyo mgonjwa. Na hata barabara zetu ni mbaya sana tafadhali tuangaliwe na njia zote katika katiba inayokuja. Nikimalizia kidogo niseme kama mtu wa karo niliwambia mimi ni mtu wa kario. Nitazungumza kidogo kwanza niseme kiswahili nilisikia kwa kiswahili watu wanasema nisemwapo ulipo na kama halipo laja. Tumewai kusikia kwamba wale wazee

wameretire kutoka kwa serikali, anyway ni kusikia tu hatuwezi kujua ukweli wake lakini uenda kama ni hiyo. Tunasikia kwamba wazee hawa wakifikia maumri Fulani yale malipo yao yataondolewa ama mtu akifikia maumri Fulani malipo yake yanaondolewa . Ssa niulize mtu akiwa mzee sana ndio anahitaji kusaidiwa ama kama ako na nguvu kidogo? Ni afadhali mimi naona mtu huyu aendelee kusaidiwa na hayao malipo yake kidogo kidogo mpaka Mungu atakapomwondoa kwa sababu Mungu hajafanya makosa kumpa huyu umri kubwa. Tafadhali sana jambo hilo iangaliwe na katiba itakayokuja. Nafikiri hii ni mezungumzia mengi kuhusu elimu, ningeomba tena hapo kuongeza katika sehemu Fulani kama hizi zetu tuwe na mashule za walemavu nyingi. Kwa mfano hapa watu wlemavu huenda safari ndefu sana kutafuta shule ama wazazi hutafuta shule kwa njia ngumu sana. Ziwe karibiu karibu kama district iwe na shule kama ya wasioona na wale wengine wasiosikia na wale wengine wasiotembea sawasawa ili kupunguza garama ya usafiri maanake hata hiyo imepanda sana kwa wazazi na hata kwa watoto wenyewe. Kwa hivyo kufikia hapo sina mengi isipokuwa nawashukuru sana kwa kuwa maoni hayo nafikiri yatakutana na mengine ambayo labda kutoka kwa watu wengine ambao wameona shida kama hizi, ambazo nimeongea juu yake. Asanteni9 sana.

**Com. Zein:** asante bwana Joseph. Usiondoke kaa hapo hapo, kuna swali pengine anataka kukuliza commissioner. Nilikupa muda maratatu ya wale wenzako kwa sababu mara nyingi watu walemavu hawapewi fursa ya kutosha kwa hivyo sikumharakisha kwa sababu hiyo. Watu wasione kwa nini sikumharakisha kwa sababu walemavu wanapewa fursa chache sana kulingana na wanacnhi wengine katika nchi yetu. Kwa hivyo kama tume tunatoa fursa kubwa kwa walemavu na watu wengine ambao kihistoria wamekuwa hawana fursa ya kutosha.

**Com. Ratanya:** asante sana bwana commissioner. Bwana Joseph Nyaga kuna pahali umeguzia kuhusu pension, kwa sababu umesema wewe ni mtu wa karo, pension

**Mr Nyaga:** ndio

**Com. Ratanya:** Hapo mambo ya pension vile ninavyojua utaendelea kupata pension mpaka maisha yako yote kulingana naq katiba tunayo sasa, ile current constitution ambayo tunarenew. Pengine ukisikia kwa rumour, pengine inawez a kuonolewa ukiwa tu unaendelea kuishi lakini ninavyojua kulingana na katiba ile iko,hiyo pension payment, hiyo kitu kidogo ambao wazee wanalipwa hata mimi, ni retired na ni mtu wa pension

**Mr Nyaga:** ndio

**Com. Ratanya:** utaendelea kulipwa mpaka maisha yako lakini yale anasemwa sana bwana Nyaga ni kwamba wazee wanauliza sana hiyo kitu ikwa inaongezewa wakati wengine wameongezewa, si ndio?

**Mr Nyaga:** ndio

**Com. Ratanya:** mshahara ukiongezwa wa public officers na wao wanaongezewa.

**Mr Nyaga:** ndio

**Com. Ratanya:** hiyo ni maoni ya wazee retired kila pqahali. Hata mimi. Hata hiyo unasema ni mzuri?

**Mr Nyaga:** ni muhimu sana kwa sabanu—

**Com. Ratanya:** hiyo tumekubaliana. Thank you very much.

**Com. Zein:** bwana Joseph subiri hapo italetwa uchukuliwe jina lako kwamba umetoa maoni kwenye kitume wa kurekebisha katiba.

**Mr Nyaga:** asante.

**Com. Zein:** Sasa tunamwita Daniel Njagi. Karibu mzee.

**Daniel Njagi: in vernacular**

**Interprator:** mimi ni Daniel Njagi

**Mr Njagi:**

**Interprator:** anaona ya kwamba mambo yameharibika na atazungumzia juu ya mashamba.

**Mr Njagi:**

**Interprator:** kwa sababu zamani

**Mr Njagi:**

**Interprator:** kukazana kulikuwa ni mtu ametoa yale mawe ya mpaka.

**Mr Njagi:**

**Interprator:** hakukuwa na huduma ya kugawanya mashamba

**Mr Njagi:**

**Interprator:** na kama ingekuwa ya kwamba nimeondoa jiwe la mpaka

**Mr Njagi:**

**Interprator:** yule ambaye tumepakana naye

**Mr Njagi:**

**Interprator:** alikuwa anaitwa wazee

**Mr Njagi:**

**Interprator:** na mimi ninaita wazee wangu

**Mr Njagi:**

**Interprator:** wazee hao

**Mr Njagi:**

**Interprator:** wake pekee na wangu pekee yake walikuja pamoja

**Mr Njagi:**

**Interprator:** walifanya case na hawa wzee

**Mr Njagi:**

**Interparator:** yule angashindwa

**Mr Njagi:**

**Interprator:** waliulizwa wanywe yale kiapo ya kienyeji

**Mr Njagi:**

**Interprator:** hapo hapo

**Mr Njagi:**

**Interprator:** mtu alitoa (ndegwa) ni n'gombe dume

**Mr Njagi:**

**Interprator:** na akatoa mbuzi

**Mr Njagi:**

**Interprator:** sasa wakala kile kiapo

**Mr Njagi:**

**Interprator:** kwa wazee hawa ndio waliona kwamba nani alishinda katika ile kesi.

**Mr Njagi:**

**Interprator:** kama ilikuwa ni mambo ya mashamba wote kila mmja alitoa katika lile shamba ambalo alikuwa anasaema ni lake.

**Mr Njagi:**

**Interprator:** hawa ndio waliwafanya wakasikizana

**Mr Njagi:**

**Interprator:** ikitoka pale

**Mr Njagi:**

**Interprator:** hapo waliambiwa yule aliyekuwa amepatikana na makosa amlipe yule mwingine

**Mr Njagi:**

**Interprator:** na mwaka wa 1972,

**Mr Njagi:**

**Interprator:** hapo ndipo mambo yalianza kuharibika

**Mr Njagi:**

**Interprator:** juu ya mashamba

**Mr Njagi:**

**Interprator:** sasa mambo yote yamekuwa yakiendelea kwa karamu tu na mfuko, yaani pesa.

**Mr Njagi:**

**Interprator:** kwa sababu watu wamekuwa wakihongana.

**Mr Njagi:**

**Interprator:** yule mtu ambaye hana nguvu

**Mr Njagi:**

**Interprator:** hata kama ni mahali pake ilikuwa inachukuliwa inaenda

**Mr Njagi:**

**Interprator:** yeye anaunga mkono ya kwamba warudie yale mambo ya kienyeji ya kukula kiapo ili mtu anaweza kusema juu ya mashamba yake ama shamba lake

**Mr Njagi:**

**Interprator:** kitu kingine

**Mr Njagi:**

**Interprator:** ni juu ya uchaguzi

**Mr Njagi:**

**Interpreter:** kama mtu anataka kuwa mkubwa

**Mr Njagi:**

**Interpreter:** anafaa kufuatwa kimlolongo

**Mr Njagi:**

**Interpreter:** hata kama ni chief

**Mr Njagi:**

**Interpreter:** hata kama ni assistant chief

**Mr Njagi:**

**Interpreter:** anaonelea kwamba kufuatana ndiko kutakuwa ni kuzuri

**Mr Njagi:**

**Interpreter:** anaona ya kwamba yule anatakaye kuchaguliwa ama kupewa kazi yoyote awe ni mtu mwenye shamba kwa sababu akiwa hana shamba anarudi kufanya njama ya kudanganya wengine yale mashamba yao.

**Mr Njagi:**

**Interpreter:** ndio hio, asante.

**Speaker:** asante sana. Ngojewa subiri, commissioner anataka kukuliza swali.

**Com. Ratanya:** ningetaka kuliza mzee Daniel hapa afafanue kitu kimoja nataka kujua, na hicho ni kwamba hii noti ama emetamuma (**continues in vernacular**) kaurugo. Hiyo ni oath ya kiapo kimbeere. Thank you very much.

**Robert Njuki: in vernacular**

**Interpreter:** anasema mimi ninaitwa Robert Njuki na

**Mr Njuki :**

**Interpreter:** mimi shida ambao ninaiona na naweza kusema ni hii

**Mr Njuki:**

**Interpreter:** watu wanasumbuliwa sana na maji ya kuteka

**Mr Njuki:**

**Interpreter:** kuna watu ambao wako na pipes kule nyumbani na kuna wengine hawana mtu anaweza kuteka tuseme mitungi kumi

**Mr Njuki:**

**Interpreter:** mtu akiteka mitungi kama kumi hivi huwa usiku anachoka sana

**Mr njuki:**

**Interpreter:** kila mtu inampasa awe na majia uko kwake nyumbani

**Mr Njuki:**

**Interpreter:** kitu cha pili

**Mr Njuki:**

**Interpreter:** ningependa tu kusisitiza juu ya mashamba

**Mr Njuki:**

**Interpreter:** watu waangaliwe sana juu ya mashamba

**Mr Njagi:**

**Interpreter:** kwa sababu watu wengine wananyan'ganya wengine kwa sababu ya pesa.

**Mr Njuki:**

**Interpreter:** na shida zote hizi kwa kimbere zinaweza kumalizwa na kaurugo tu

**Mr Njuki:**

**Interpreter:** mimi mambo yangu ambaye nilikuwa nayo ni kama hiyo tu, asante

**Speaker:** asante sana mzee kwa hayo uliyotupa. Tafadhali uende pale uandike jina ile register, asante sana. Victoria Ndegi, karibu dada.

**Victoria Ndegi:** asante sana. Kwa majina ni Victoria Ndegi. Yangu ni memorandum tatu. Moja nilitumwa na gikundi kinaitwa Karie women group. Yapili ni mtu mmoja ako nyumbani anaitwa Benard Nyaga na hana macho. Yake ndio nimesoma , hiyo ingine mbili nipeane. Na imeandikwa na kimbeere.Na nilisona kama hivyo ilikuwa inaandikwa. -----

**(inaudible)**

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** shida ya mtu ambaye haoni

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** ni nguo

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** ni chakula

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** kuna mtu aliyezaliwa bila macho lakini hana mama hana baba

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** mtu kama huyo anasumbuka sana

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** zaidi mno ni kwanza kuna watoto wachanga

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** na wengine hawaoni na wengine ni walemavu hawana miguu

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** anauliza

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** wakati wa kurekebisha katiba hii

**Madam Victoria:**

**Interpreter:** watu hawa watayarishiwe au watengenezewe shule kila pahali

**Madam Victoria:**

**Interprator:** kwa hivyo

**Madam Victoria:**

**Interprator:** kama katiba ingerekebishwa ili kuweza kusaisia watu kama hao ambao hawana miguu wala hawana macho, angeshukuru sana

**Madam Victoria:**

**Interprator:** yeye amesema jina lake ni Benard Nyaga Kinaino

**Madam Victoria:** asantesana

**Interprator:** na ile ingine anaileta

**Com. Zein:** asante sana Victoria kwa hayo maoni yako. Kwa hivyo peana na uweke sign kwa register wetu. Sa sa tungeendelea kwa Juliana Machoni. Huyu Juliana ni kusikiliza tu. Tuna Isaac Machaki Mwea. Sasa ni wakati wako.

**Isaac Machaki Mwea: in vernacular**

**Interprator:** anasema ni asante sana kiongozi.

**Mr Machaki;**

**Interprator:** ninaitwa Isaac Machaki

**Mr Machaki:**

**Interprator:** kwetu ni karangare

**Mr Machaki:**

**Interprator:** na kama utakuwa ninmakosea ni kwamba nina homa

**Mr Machaki:**

**Interprator:** maoni yangu

**Mr Machaki:**

**Interprator;** ile ambayo imenileta hapa

**Mr Machaki:**

**Interprator;** sisi tumesukumwa sana tukiwa mbeere

**Mr Machaki:**

**Interprator:** watoto wetu hawajiriwi

**Mr Machaki:** kutoka nursery

**Mr Machaki:**

**Interprator:** mtoto anasoma mpaka kidato cha nne

**Mr Machaki:**

**Interprator:** anakuja nyumbani anakaa

**Mr Machaki:**

**Interprator:** sasa baba yake amawacha bila chochote

**Mr Machaki:**

**Interprator:** hata shamba aliuza



**Mr Machaki:**

**Interprator:** mimi naomba hii katiba

**Mr machaki:**

**Interprator:** watoto wa mbeere waweze kuajiriwa

**MrMachaki**

**Interprator:**wale ambao masomo yao ni mazuri

**Mr Machaki:**

**Interprator:** hiyo imekwisha

**Mr Machaki:**

**Interprator:** ya pili ni hivi

**Mr Machaki:**

**Interprator:** haya mashamba yote ambayo yamezungumzwa, tangu nikuje hapa imekuwa yakitajwa tajwa.

**Mr Machaki:**

**Interprator:** kuna shida

**Mr Machaki:**

**Interprator:** ninamuliza namuzia huyu jamaa shamba?

**Mr Machaki:**

**Interprator:** na hata hatuna mpaka na yeye

**Mr Machaki:**

**Interprator:** na yeye akauzia mwingine

**Mr Machaki:**

**Interprator:**yule ambaye amepakana na yeye hajui

**Mr Machaki:**

**Interprator:** katiba hii ningependa iseme hivi

**Mr Machaki:**

**Interprator:**hakuna mtu ambaye angeweza kuuza shamba lake kama yule waliyena mpaka na yeye hayuko

**Mr Machaki:**

**Interprator:** huo ni uizi

**Mr Machaki:**

**Interprator:** kama ikiwa ni kwa sababu ya karamu imeandikwa kwa karamu

**Mr Machaki:**

**Interprator:** ya tatu

**Mr Machaki:**

**Interprator:** sisi tukiwa wa mbeere

**Mr Machaki:**

**Interprator:** tulikuwa na laana

**Mr Machaki:**

**Interprator:** kwa sababu ukimwi

**Mr Machaki:**

**Interprator:** umeletwa na watu

**Mr Machaki:**

**Interprator:** na hawa watu wanafundishwa

**Mr Machaki:**

**Interprator:** anasema kwa kimbeere kwamba mwili wa mwanamke, msichana haukuonekana hakuwaunaonwa tu.

**Mr Machaki:**

**Interprator:** sasa yule mwana mwali ndiye anavaa kama mama yake

**Mr Machaki:**

**Interprator:** anasema ya kwamba kamisi ya mama ambaye ni mzee haikuweza kuonekana na mtoto ambaye hana mtoto mwingine amezaliwa nhyuma yake.

**Mr Machaki:**

**Interprator:** Katika hii kigeuzo

**Mr Machaki:**

**Interprator:** hiyo mambo ya --- (inaudible) sana

**Mr Machaki:**

**Interprator:** kila mama ana nguo yake.

**Mr Machaki:**

**Interprator:** kuna nguo ya msichana ambaye hajaolewa na mama

**Mr Machaki:**

**Interprator:** wakati katiba hii itarekebishwa, mambo haya yaangaliwe vizuri sana

**Mr Machaki:**

**Interprator:** ninaona aibu sana kwa sababu wale watu ambao wanasema Yesu ni mwokozi ndio hawa wamepasiliwa nguo zao huko nyuma.

**Mr Machaki:**

**Interprator:** sitaji kusema mengi kuliko hiyo.

**Mr Machaki:** thankyou

**Interprator:** asante sana

**Com. Zein:** ok asante sana bwanaq Isaac kwa hayo maoni yako. Kwa hivyo unaweza kupeana memorandum yako kama iko, kama haiko weak sign kwenye register yetu. Asante sana. Na hapo kuna mwingine ambaye anaitwa A N Mugo. Kama Mugo hayuko tutaenda kwa Pastor J Munyi. Hata pastor Munyi hayuko. Frida W--. Pastor yuko karibu? O k pastor endelea.

**Pastor John Munyi:** asante sana. Mimi ndiye pastor John Munyi. Nina maoni kuhusu kanisa.

**(Interjection):** shika vizuri namna hiyo

**Pastor Munyi:** makanisa yetu ya kiroho, hasa sisi tunatawaliwa na roho mtakatifu, ningeliomba katika katiba hii letu la Kenya. Pahali popote patakuapo na kesi yoyote, manabi wale ambao wamepewa vipawa na mwenyezi Mungu wae wakiulizwa mahali popote watu watakuwa wakileta mufurugano, maana vipawa zake Mwenyezi Mungu yuko. Natoka mahali pa --- **(inaudible) unaendelea pahali pengine**

**(Interjection from the speaker):** umemaliza?

**Pastor Munyi:** eh hapo nimemaliza

**Speaker:** kanisa lako linaitwaje?

**Pastor Munyi:** The Gospel of God's Church

**Speaker:** ok, asante sana John

**Pastor Munyi:** jambo lingine la pili

**Speaker:** sema yote. Uko na dakika tatu imebaki.

**Pastor Munyi:** haya. Kuhusu uchaguzi tunaochaguana our members of parliament, tuliwachagua ni wanze kutoka grassroot kufanya kazi mpaka mwisho kwa president. Wakifanya kwa president mradi yoyote ikikuja, akuje nayo mpaka chini mpaka mahali sub-location iko. Ndio donors wote watakaoleta msaada wowote isipotelee njiani. Ikipitea sisi ambao tumemchagua tutampata an tutafuta kiongozi mwingine atakuako na mienendo ilioko mzuri. Kama hataweza kufanya kazi mzuri vile tumemtuma. Na jambo lingine president naye pia apewe mamlaka yana uzito. Aw akikalishwa chini pia na wanabii wakiwapo karibu ndio mambo yakikuja mrama, atakuwa aki---(inaudible) kulingana na vipawa ambao tumepewa tumetoka. Kwa jua kali, wanajua kali nao wapewe mamlaka yafaavyo mali yao ichunguluwe sawasawa isje kwa mifuko ya wachache wanaojipenda zaidi. Maana wanawajua kali hatupewi nafasi vizuri. Mali ikkuja inapotelea njiani, haifikii wale qambao wanaohusika katika grassroot. ----- (inaudible)

**Com. Zein:** ok pastor John Munyi kam umemaliza ni sawasawa, enda hapo uweke sign. Asante sana pastor Munyi. Then kuna Fridah David Njeru. Sasa ni wakiati wako Frida

**Frida W Njeru:** asante sana bwana commissioner. Maoni yangu ni machache. Majina ni kama mmetaja Frida Wangeri Njeru. Kwanza nitazungumzia juu ya jamii. Ninaonelea kuwa kama mume na bibi wanafikia kiasi ya kuwachana, mali ambaye wamepata kwa huo muda wamekuwa wamekaa pamoja igawanywe kati yao wawili. Hii ni kwa sababu wanawake wamekuwa wanatupwa na mabwana zao kama vile walikuwa wameenda huko na kulala tu. Na pengine wamechangia kwa kiasi kikubwa kupata hiyo mali ambao wako nao. Mimi naona katiba ikitengenezwa, mali kati ya bibi na bwana kama wanaachana igawanywe kati ya hawa wawili. Kuhusu mashamba wanawake wamekuwa pia hawana kitu kuhusu mashamba. Maoni yangu ni kuwa, wanawake wamekuwa nyuma kwa jambo hili. Kama wasichana wetu tunawapa elimu sawa na wavulana. Ikifika kwa mashamba hawana chochote. Maoni yangu nikuwa hata mashamba woa wanapatiwa na baba zao kama vile elimu. Na wale wanawake ambao wameolewa pia wawe wanahusika katika tittle deed kwa mashamba yao. Kama zile ikiwa ni bwana na bibi tittle deed iwe na majina yao wakiwa wawili. Hii ni kwa sababu wakati mwingine bwana akiaga dunia, bibi anaachwa nyuma akiteseka sana kwaw kutrafuta ile njia ambaye anaweza

kugawana ile shamba lao kati ya watoto wao. Ya tatu ni kuhusu elimu ya chuo kikuu. Hii imekuwa ni ngumu sana na tunaendelea kuwapeleka watoto wetu shuleni. Lakini wengi wanafika hapo unaona wazazi hawawezi. Ninaonelea kwamba elimu ya vcioo vikuu iwe ya bure kama ilivyokuwa huko mbeleni. Ya nne na ya mwisho, ni kwamba wale wanaume ambao wanawanyasya wanawake wachukuliwe hatua. Asante.

**Com. Zein:** ok asante sana fridah kwa hayo maoni yako na anayefuata sasa ni Humphrey Njoka.

**Humphrey Njoka:** asante, kwa jina mimi naitwa Humphrey Njoka. Maoni yangu ya kwamba mimi naona hii pesa ya karo ya shule, hiyo katiba irudishe pale ilikuwa mbeleni. Kwa maana tukiangalia huko gishagi huko watu wako nja watoto wengi sana hawaendi shule. Kwa maana sasa kama sisi hapa wa mbere ni watu wa kufuga. Tena na mali tunafuga hapa kama n'gombe hakuna n'gombe inawezatokea ngiri kumi. Na tena hata vichaka tuko naye huko, huwezi fuga n'gombe kama kumi hivo. Sasa hata mtoto akienda shule, unaona tu mtu kwa maana hakuna kazi anafanya isipokuwa kutegemea hiyo mifugo yake lazima auze ile n'gombe yake. Tena hapa sisi ni watu wanakaa kama watu wako janguani, jua ni kali. Tunaona tu mimiea mara moja kwa miaka. Ssa unaenda tu unauza ile n'gombe yako inatoka kama elfu tatau unapeleka shule yote. Sasa ikiangalia wengine huko watoto hawana nguo, umepeleka mtoto kwa shule. Tena wakati umepeleka mtoto shule anakula pesa yote na kuna wengine wako nyuma. Sasa ukiangalia hawa wako nyuma yule mtoto ambaye amemaliza shule amemaliza kusoma na hajapata kazi. Sasa wewe mzee ukiwa nyumbani unaangalia tu unaona kweli hata kupeleka huyu mwingine shule tu ni kazi bure afadhali ukae namna hiyo kwa maana ukimpeleka shule hakuna usaidizi anakusaidia nao. Umemsomesha halafu tena anarudi nyumbani. Sasa si unaona hapo kweli hauna usaisizi. Haya ya pili, hospitali kweli watu wanasumbuka sana. Kwa maana unatoa mtu yako nyumbani akiwa mgonjwa unampeleka hospitali. Hii cadu unaenda kutoa ya kwanza ni pesa. Tena wewe ni mtu wa huko oko na siku mingi bila kupata pesa. Haya bahati mbaya mtu wako aende aage dunia.

**(Interjection):** kwa hivyo kwa hospitali ungependekeza nini?

**Mr Njoka:** kwa hospitali tuwache kulipishwa pesa.

**Com. Zein:** ok

**Mr Njoka:** Haya hii mashule naye tuko na mashule mengine wako kichakani huko sana na tena tuko na watoto wanasomea huko. Hatuna kama kitu agent kama simu. Mtoto anaweza ngonjeka kibahati mbaya na sasa mtoto akingojeka kama huko Irira anatolewa huko na baiskeli analetwa hospitali. Sasa mimi naomba tupeleke masimu kwa shule kwa maana mtoto akingojeka unaweza piga simu gari inakuja kwa haraka anachukuliwa. Sasa mimi naomba hapo tuangaliliwe. Masimu tupewe kwa mashule na bara bara mzuri. Haya hapa pengine watu kama mimi ni wengi ambao wamesoma hapa mbele na hatupati kazi. Kama umesoma unaenda mbele unaenda kama interview ikifanywa ya polisi, unaenda unaitishwa elfu kumi. Sasa kama pahali umeto0ka huwezi hata ona elfu tatu. Hii kazi ya hongo naye imeleta noma kwa maana sasa kama umeenda kufanya interview na huna kitu, hata ukiwa tu unafanya kwa mlolongo tu ukiwa unakimbia huko ukweli inaonekana hata ufaulu huwezi ukachukuliwa kwa maana haujatoa kitu. Tena wewe unarudi kuwa makanga. Ukija kufanya makanga asiye makanga, tena kila wakati unakamatwa tu bure ati wewe ni makanga mtu wa harimu. Na vile imefanya wewe uwe makanga ni kwa kuwa umesoma na hakuna kazi ingine unawezafanya. Kwa hivyo hapo mahali tuangaliliwe. Sina mengi ni hayo tu.

**Speaker:** asante sana bwana Humphrey Njoka na tena tuna Daniel Nguo. Daniel yuko hapa karibu. Haya kama Daniel yoko hapa ni wakati wako sasa.

**Daniel Nguo:** in vernacular

**Interprator:** mi naitwa Daniel Nguo. Mr Nguo:

**Interprator:** wa Kanyenyeo

**Mr Nguo:**

**Interprator:** maoni yangu

**Mr Nguo:**

**Interprator:** ninasema hivi

**Mr Nguo:**

**Interprator:** anauliza kama mto kunapitia hapo unaitwa dhoch kama kuna wakati unakauka

**Mr Nguo:**

**Interprator:** anauliza sababu ni hii

**Mr Nguo:**

**Interprator:** mvua

**Mr Nguo:**

**Interprator:** mvua imepotea.

**Mr Nguo:**

**Interprator:** nilikuwa nasema hivi

**Mr Nguo:**

**Interprator:** maji ile ambayo yaliyokutoboa

**Mr Nguo:**

**Interprator:** ifunguliwe

**Mr Nguo:**

**Interprator:** tulime na hiyo maji ya irrigation ama ya msingi.

**Mr Nguo:**

**Interprator:** maanake hiyo haitaisha huku mbeere

**Mr Nguo:**

**Interprator:** yeye anaitwa Nguo alikuwa huko Misri wakati wa vita

**Mr Nguo:**

**Interprator:** alikuwa katika vita mwaka wa alfu moja, mia tisa na arobaini na moja

**Mr Nguo:**

**Interprator:** na hiyo shida anaopata mpaka wakati huu.

**Mr Nguo:**

**Interprator:** hajapewa retire aliachiliwa hivo tu.

**Mr Nguo:**

**Interpreter:** hata sasa

**Mr Nguo:**

**Interpreter:** tunaomba ya kwanza katiba iweze kuruhusu ama kufanya uwezekano ya watu wote kulima kwa maji, hii majui ya irrigation

**Mr Nguo:**

**Interpreter:** maoni yangu ni hayo tu sina ingine

**Com. Zein:** mwambia mzee asante sana

**Interpreter:** aandiki

**Com. Zein:** nani wacha mzee akae tu. Pelekea yeye register pale

**K. Kanyiva: in vernacular**

**Interpreter:** mimi naitwa K Kanyiva

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** mimi nimeleta mambo kuhusu mashamba

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** kwa sababu kutoka mwaka wa alfu moja mia tisa na sabini

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** ndio wakati mashamba ya hapa mbeere imekuwa na shida

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** wakati wa kugawanywa

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** kumekuwa na watu wengine ambao wamesababisha hizi shida

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** mtu alipopata lile shamba

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** na namba yake

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** wale watu waliyo na pesa

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** waligeuza zile namba za wale watu wakapata tittle

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** kama ingewezekana

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter:** mashamba haya yawekwe kwa computer ili mtu akishapewa shamba lake iwe katika computer

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** watu wengine wameingilia wengine kwa sababu ya pesa

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** ikiwezekana

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** utamaduni ya kimbeere

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** ni wale ile kiapo ya kimbeere

Mr Kanyiva:

**Interprator:** hiyo ndio inaweza kuwatenganisha

**Mr Kanyiva;**

**Interprator:** kwa sababu katiba hii ni ya kusaidia

**Mr Kanyiva;**

**Interprator:** kuangalia mambo hayosana

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** kwa sababu pahali tumefika

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** inaweza kuleta mfarakano hata mauaji

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** mahsamba

**Mr Kanyiva:**

**Interprator;** ni kama mwili

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** ukiguza mwili wa mtu

**Mr Kanyiva;**

**Interprator:** anasikia chungu mahali pote

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** hiyo ndio nilikuwa nataka kuzungumzia

**Mr Kanyiva**

**Interprator:** watu wapewe hiyo kiapoinaitwa kaurugo kwa kimbere waweze kumaliza uzia

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** kitu cha pili

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** hospitali zijengwe katika villages, manyumani pale

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** kwa sababu yale magonjwa yamo

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** si lazima apelekwe Nairobi kwa sababu ina dawa, dawa inaweza pelekwa huko

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** hiyo ndoi kitu ingine

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** cha tatu

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** sijasikiaikisemwa

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** yule mwalimu wa nursery

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** aangaliuwe sana

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** kwa sabau kabla mtoto hajaelimika

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** ni mwalimu wa nursery ndiye anafanya mtoto kuelimika

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** walimu wa nursery school si lazima wapew mshahara na wazazi

**Mr Kanyiva:**

**Interprator;**hata mwalimu wa nursery aajiriwe na serikali

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** kwa hivyo katiba hapo iangalie sana

**Mr Kanyiva:**

**Interprator:** jambo la nne

**Mr Kanyiva:** kuna mtu mwingine yuko hapa

**Mr Kanyiva;**

**Interprator:** subarea

**Mr Kanyiva:**

**Interprator;** yeye pia anasaidia serikali

**Mr Kanyiva:**

**Interprator;** yeye anafaa kuangqaliwa apewe kitu kidogo

**Mr Kanyiva:**

**Interprator;** na kama hawezi kuajiriwa kwa mshahara basi afanyiwe harambee

**Mr kanyiva:**

**Interprator;** kwa sababu anasaidia assistant chief na chief



**Mr Kanyiva;**

**Interpreter;** hata na serikali yenyewe

**Mr Kanyiva :**

**Interpreter;** kwa hivyo mimi sina mengi

**Mr Kanyiva;**

**Interpreter:** ni hayo asante

**Mr Kanyiva:**

**Interpreter;** Mungu awasaidie

